

MKATABA WA UPANGAJI WA VYUMBA LODGE

Makubaliano haya yamefanyika leo tarehe 04 ya mwezi wa February Mwaka 2025

KATI YA


Bw EDWARD B. MAKWETA wa S.L.P 410, MAKAMBAKO, NJOMBE, TANZANIA, ambaye ni Mmiliki wa IDDY MT. LODGE iliyopo Kitongoji cha Nyanyanjo Mtaa wa Igomelo, Kata ya Lugelele, Wilaya ya Mbarali Mkoa wa Mbeya, katika mkataba huu atajulikana kama **MPANGISHAJI**

NA

JANDU PLUMBERS LIMITED wa S.L.P 409, ARUSHA, TANZANIA mwenye akili timamu mkazi wa UNGA LIMITED, ARUSHA ambaye katika mkataba huu atajulikana kama **MPANGAJI**

MAKUBALIANO KATIKA MKATABA HUU ni kama ifuatavyo:

1. Kwamba Mpangishaji anapangisha Lodge hiyo na pia mpangaji anahitaji Lodge hiyo kwa ajili ya Malazi kwa kuzingatia vigezo na masharti yaliyoanishwa kwenye mkataba huu.
2. Kwamba, mpangishaji amekubali kupangisha Lodge hii kwa kipindi cha miezi kumi kuanzia tarehe 04 February 2025 hadi tarehe 03 November 2025.
3. Mpangaji atalipia jumla ya vyumba Kumi na Moja.
4. Kwamba Makubaliano ya Kodi ya Lodge kwa mwezi ni kiasi cha Tsh 3,470,000 (Shilingi Million Tatu Laki Nne na Efu Sabini), na kata 10% ya With Holding Tax na lipa TRA.
5. Kwamba Mpangishaji anakubali kutokodisha sehemu yoyote ya mali ndani ya mipaka ya Lodge hii ya kulala wageni kwa wengine wowote. Mpangaji amejiri mali yote isipokuwa vyumba 3 kati ya vyumba 14. Vyumba hivyo 3 vitafungwa na mpangaji hana njia ya kufikia isipokuwa amekubaliana na Mwenye Nyumba kwa maandishi.
6. Kwamba Mpangaji atalipa kiasi cha Tsh 3,470,000 (Shilingi Million Tatu Laki Nne na Efu Sabini) mnamo tarehe 05 February 2025 na tarehe 25 February 2025 atamalizia kiasi cha Tsh 6,940,000 (Shilingi Million Sita Laki Tisa na Efu Arobaini tu) ambayo itakuwa ni malipo ya kodi kwa kipindi cha miezi Tatu. Kodi zaidi italipwa kwa kila miezi mitatu mapema.
7. Kwamba, kodi ya Lodge hiyo italipwa kupitia akaunti ya benki ya mpangishaji ambayo ni:
Jina la benki : **NMB**
Akaunti namba : **62210012868**
Jina la Akaunti : **EDWARD BATHROMEO MAKWETA**
Aina ya Akaunti : **Tanzania Shilingi**
8. Mpangishaji atamkabidhi mpangaji Lodge hiyo baada ya pande zote kusaini mkataba huu tarehe husika pamoja na malipo kukamilika kama ilivyoainishwa kwenye kipengele namba 5 hapo juu.
9. Kwamba Mpangaji na Mpangishaji wamekubaliana kuwa Mpangishaji anachukua jukumu la kutoa huduma za usafishaji wa vyumba, bafu, sehemu ya kulia chakula na maeneo ya nje ya Loji ikiwa ni pamoja na bustani, kufua na kupiga pasi nguo, kutoa ulinzi kwa muda wote wa upangaji wake.
10. Kwamba, Mpangaji atawajibika kwenye gharama za umeme kwa kipindi chote cha mkataba huu.
11. Kwamba, endapo mpangaji ataharibu kitu chochote kwenye Lodge hiyo ndani au nje atatakiwa kutengeneza au kulipa gharama za matengendo ya kitu kilichoharibika na kuvirudisha katika hali yake ya mwanzo (EXCEPT FOR BATH SYSTEM, CEILING AND TILES).
12. Kwamba, Mpangaji haruhusiwi kupangisha lodge hiyo au sehemu ya lodge hiyo kwa mtu mwingine bila ridhaa ya mmiliki.
13. Kwamba, Mpangaji atatakiwa kutoa taarifa ya kuongeza au kutokuongeza mkataba mwingine baada ya kipindi cha mkataba huu kukamilika au kuisha kwa kwa ajili ya ukaguzi pamoja na marekebisho madogo madogo yatakayoonekana.



14. Kwamba, mpangaji atachukua tahadhari ya kutosha dhidi ya jambo lolote linaloweza kuhatarisha usalama wa Lodge hiyo kama moto.
15. Mpangishaji atawajibika na madai yoyote yatakayojitokeza, kupinga mamlaka ya Mmiliki kupangisha pango hilo.
16. Kwamba, endapo mtu yeyote atafanikiwa kupinga uahalali wa mamlaka yake ya kupangisha Lodge hiyo mbele ya vyombo vya sheria na Mpangishaji atarejesha kwa Mpangaji fedha zote za thamani ya upangishaji utakaokuwa umebaki kwa wakati huo.
17. Kwamba, mpangaji atapewa notisi ili kuweza kumruhusu mwenye nyumba au muwakilishi wake kuweza kukagua hali ya nyumba na mazingira yanayoizunguka au kufanya matengenezo endapo yatahitajika.
18. Kwamba, mpangaji atapewa notice ya siku tatu endapo atakiuka moja ya makubaliano ya mkataba huu na kushindwa kurekebisha kwa kipindi cha siku tatu. Makubaliano haya yanefanyika mbele ya mashahidi wa pande zote mbili katika tarehe na mwaka kama ilivyooneshwa kwenye mkataba huu.

IMESAINIWA NA (Mpangishaji)

Jina : EDWARD BASHAROMBO MOKWETA

Saini : [Signature]

Namba ya simu : 0769 800819

Mbele ya (shahidi)

Jina : BOB MOHAMED NIKATA

Saini : [Signature]

Namba ya simu : 0743 584 288

Leo tarehe 04 Mwezi February Mwaka 2025

IMESAINIWA NA (Mpangaji)

Jina : RAMNADH R. KOTTURU

Saini : [Signature]

Namba ya simu : 0717 718 719

Mbele ya (shahidi)

Jina : GURVEER SINGH

Saini : [Signature]

Namba ya simu : 0759385466

Leo tarehe 04 Mwezi February Mwaka 2025